

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOLO



Kumb. Na. KDC/AB/41/01

20/02/2018

TANGAZO LA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo amepokea Kibali cha Ajira chenye Kumb Na: FA/71/363/01/38 cha tarehe 31/07/2017 pamoja na Kibali Kumb. Na: FA/170/363/01/48 cha tarehe 22/09/2017. Aidha kufuatia vibali hivyo Mkurugenzi Mtendaji (W) anawatangazia wataanzania wote wenye sifa za kujaza nafasi za kazi kama ifuatavyo:-

1. KAZI: MTENDAJI WA KIJIKI DARAJA II (Nafasi 1)

SIFA ZA MWOMBAJI

Awe amehitimu mafunzo ya Stashahada/Diploma katika mojawapo ya fani zifuatazo: Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka katika Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo Dodoma au Chuo chochote kinachotambulika na Serikali.

MAJUKUMU YA KAZI

- Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji
- Atakuwa Katibu wa Kamati/Mikutano ya Kijiji
- Atakuwa mlinzi wa Amani na Msimamizi wa Utawala Bora katika Kijiji
- Ataratibu na kusimamia upangaji wa utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Kijiji
- Kutatafsiri na kusimamia Sera, Sheria na Taratibu
- Kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji mali.
- Kiongozi wa wakuu wa vitengo vya kitaalam katika kijiji
- Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za kijiji.

NGAZI YA MSHAHARA NA MSHAHARA WA KUENZIA

TGS C1 = TSHS.525,000/= Hadi Tshs. 668,000

